# HOTUBA YA NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA NNE (4) CHA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC – JIJINI ARUSHA,

## FEBRUARI 08, 2024

---

***Mhe. Emmanuela Mtatifikolo Kaganda,*** *Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

***Ndg. Xavier Daudi;*** *Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

***Dkt. Jasmine Tiisekwa;*** *Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Mha. Benedict Ndomba;*** *Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Bw. Said Seif Said;*** *Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

***Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,***

***Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali***

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;***

***Waandishi wa Habari,***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima, afya njema na kutukutanisha siku hii ya leo katika Kikao Kazi hiki cha Nne (4) cha Serikali Mtandao.

Kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru viongozi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na binafsi, Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali, Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao na Waandishi wa Habari kwa kutenga muda wenu kwa

siku zote hizi tatu (3) kwa ajili ya kushiriki katika Kikao Kazi hiki. Hii inadhihirisha ushirikiano mzuri uliopo miongoni mwetu kama wadau muhimu wa serikali mtandao, tukiwa na jukumu la kuleta maendeleo ya taifa letu, hasa kwa kutumia nyezo hii adhimu ya Serikali Mtandao.

Niwapongeze na kuwasihi kudumisha ushirikiano huu kwa mustakabali wa maendeleo endelevu ya taifa na vizazi vyetu.

Vilevile, niwashukuru Viongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), nikianza na Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti, pamoja na watumishi wote kwa moyo wao wa kujitoa na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao na kufanikisha kikao kazi hiki, pamoja na kusimamia vizuri utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma.

**Ndugu Washiriki,** napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wote kwa ushiriki wenu mzuri katika Kikao Kazi hiki ambacho tunakihitimisha leo. Nipende tu kusema kuwa, nimefarijika kwa namna mlivyoshiriki kikamilifu katika majadiliano na kutoa maoni na ushauri katika masuala mbalimbali yenye lengo la kuimarisha na kukuza jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma.

**Ndugu Washiriki,** Kama ilivyoelezwa wakati wa ufunguzi wa Kikao Kazi hiki tarehe **6 Februari, 2024,** kuwa Kikao hiki kililenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, ili

kujadiliana kwa pamoja hali ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, kuainisha changamoto na kuweka mikakati madhubuti ya kukabiliana nazo.

**Ndugu Washiriki,** nafurahi kuona kuwa Kikao hiki kimekuwa na mafanikio makubwa sana, kwani wadau zaidi ya 1,000 wa kada tofauti kutoka katika Taasisi mbalimbali za umma wameweza kushiriki, na hivyo tumeweza kupata maoni na ushauri utakaosaidia katika kukuza na kuendeleza jitihada za serikali mtandao kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma, kufanya zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

**Ndugu Washiriki,** Sitaki kurudia undani wa **kauli mbiu** ya Kikao kazi hiki inayosema ***"Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa ubadilishanaji Salama wa taarifa"*** kwa kuwa najua imejadiliwa kwa kina na kwa upana zaidi. Nisisitize kuwa, ili tuweze kubadilishana taarifa kidijitali na kwa usalama zaidi tunahitaji mipango, mikakati na utashi wa dhati ili kuhakikisha mifumo yote inayoanzishwa katika taasisi za umma inakidhi matakwa ya Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili pamoja na kuwezesha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma, pia iweze kubadilishana taarifa, huku

taarifa hizo zikiwa salama, hasa tukizingatia changamoto za maendeleo ya sasa ya teknolojia.

**Ndugu Washiriki,** Naelewa kuwa, pamoja na kujadili hali ya utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao, pia mmejadili changamoto zinazoikabili tasnia hii. Hivyo, Nawakumbusha kuwa, ili tuweze kufikia mafanikio yanayotarajiwa katika utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao, hatua na jitihada za dhati zinatakiwa kuchukuliwa ili kutatua changamoto hizo, hususani kuhusiana na misingi mikuu ya utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa ajili ya kuhakikisha matokeo yanayotarajiwa yanapatikana kwa haraka.

Katika muda wa siku tatu za uwepo kwenu hapa, mmejadiliana kwa kina juu ya changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Miongoni mwa changamoto mlizobainisha ni mifumo ya TEHAMA kutowasiliana na kuendelea kuwapo kwa urudufu wa mifumo, nafurahi kuwa changamoto hizi imebainishwa na nyinyi wenyewe ambao ni wahusika muhimu katika watekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao na Kanuni zake. Niseme kuwa, suluhu ya changamoto hizi na nyingine mlizozibainisha katika kikao hiki na kuziwekea maazimio, sasa ni jukumu la kila mmoja wetu kupitia taasisi zetu, kuziweka katika mipango ya taasisi husika ili zitatuliwe, kwa ajili ya kukuza na kuimarisha jitihada za serikali mtandao ili zisaidie katika kuboresha utendaji kazi katika taasisi zetu na utoaji wa huduma kwa

wananchi, hivyo kupelekea kufikia azma ya **Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan** ya kuwa na Serikali ya Kidijitali.

**Ndugu Washiriki,** ni jambo la kujivunia kwamba, Serikali imefanya mengi katika utatuzi wa changamoto hizi na imepiga hatua kubwa sana katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini. Lakini kwa dhati niwaombe kutatua changamoto za kiutawala ambazo ziko ndani ya uwezo wetu ambazo kimsingi hazihitaji maazimio kwani ni majukumu yetu ya kila siku.

Kama alivyozungumza **Mhe. George Simbachawene Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,** wakati wa ufunguzi kuwa zipo taasisi za umma ambazo hazijaunganisha mifumo yake ya TEHAMA na Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji taarifa Serikalini *(**Government Enterprises Service Bus - GoVESB**),* nitumie nafasi hii tena kuwakumbusha wakuu wa taasisi kuhakikisha mifumo yao inaunganishwa na kubadilishana taarifa na taasisi nyingine kama ambavyo **Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan,** amekuwa akisisitiza Taasisi za umma kuwasiliana na kubadilisha taarifa kidijitali, yaani kupitia mifumo ya TEHAMA.

Aidha, niwatake wataalamu wa TEHAMA katika taasisi zote za umma, mliopo hapa na wale ambao hawakuweza kufika katika Kikao Kazi hiki, kuendeleza ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kupitia msaada na ushauri wa kiufundi unaotolewa na e-GA, lengo likiwa ni kuhakikisha sote tunaenda pamoja ili tuweze kujenga Serikali ya Kidijitali.

Pia, niwatake Maafisa Masuuli kuweka mazingira mazuri na wezeshi katika taasisi zetu ili kufanikisha utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao. Teknolojia inabadilika kila wakati, ni wajibu wa Maafisa Masuuli kuwajengea uwezo wataalamu wenu ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia kadri yanavyoibuka. Bila kuwajengea uwezo wataalamu wetu mara kwa mara hatutaweza kufikia malengo ya kuwa na serikali ya kidijitali.

**Ndugu Washiriki,** Wizara imeyapokea maoni yote mliyoyatoa kupitia kikao kazi hiki, na itaweka mpango kazi maalum kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wake.

Vilevile, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria kuiwezesha e-GA kuendelea kusimamia kwa ufanisi unaotakiwa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

**Ndugu Washiriki,** Mabibi na Mabwana, nihitimishe kwa kurudia tena kuwashukuru kwa kushiriki, na kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuandaa Kikao Kazi hiki muhimu kilicholenga kutoa taarifa ya hali ya utekelezaji wa serikali mtandao na changamoto zake na kukubaliana hatua za kuchukuwa ili kuhakikisha tunaimarisha na kuendeleza jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma. Niwashukuru pia wageni wote waalikwa kwa kuhudhuria tukio hili muhimu.

Ni imani yangu kuwa, sote tunahitimisha kikao hiki tukiwa na uelewa sahihi na kwa mapana zaidi kuhusu wajibu wetu kama Viongozi na Watumishi wa umma katika kujenga Serikali Mtandao.

Hivyo basi, tutakapokuwa tunatekeleza jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao katika taasisi zetu, tuhakikishe pia tunazingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyopo na inayoendelea kutolewa au kuboreshwa mara kwa mara ili kuwa na matumizi salama na sahihi ya TEHAMA Serikalini.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Kikao Kazi cha nne (4) cha Serikali Mtandao kwa mwaka 2024 Kimefungwa rasmi.

***Tuijenge Serikali Kidijitali***

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**